



LOWELL PUBLIC SCHOOLS
Henry J. Mroz Central Administration Offices
155 Merrimack Street
Lowell, MA 01852

Septemba 15, 2020

Wapendwa Jamii ya Lowell Public Schools,

Tunatarajia kuwakaribisha upya wanafunzi wetu siku ya Alhamisi, Septemba 17 kwa mwanzo wa mwaka wa shule wa 2020-21. Katika ucheleweshaji katika ugavi, tuliarifiwa na muuzaji wetu kwamba mabaki ya vifaa vya kusafisha hewa tulivyoitisha awali hazitafika kama ilivyopangiwa kwa mwanzo wa siku ya kwanza ya shule. Kwa sasa, tuna vifaa 128 vya kusafisha hewa kutumiwa kote wilayani. Ili kuhakikisha usalama wa wanafunzi, familia na wafanyikazi wetu, **tumeamua awali kubadilisha mpango wetu wa kufungua upya ili kupunguza idadi ya wanafunzi wa kuhudhuria shule kibinafsi kwa mwanzo wa mwaka wa shule.** Mpango uliyobadilishwa kwa mwanzo wa shule ni kama ifuatavyo:

- Wanafunzi waliopata nafasi ya kuhudhuria kibinafsi katika shule zetu za siku - Dr. Janice Adie, Laura Lee Therapeutic na LeBlanc Therapeutic – wataripoti kwa shule hizi kwa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi, kama ilivyopangwa, siku ya Alhamisi, Septemba 17 kwa siku yao ya kwanza shuleni.
- Wanafunzi waliopata nafasi ya kuhudhuria kibinafsi katika shule zifuatazo za programu za masomo maalum ambazo zina tofauti kubwa na shule za kawaida - Classrooms for Students with Autism (Madarasa kwa Wanafunzi Walio na Usonji) (CSA), Life-skills Education and Planning (Mafunzo ya Ujuzi za Kimaisha na Mpango) (LEAP) na madarasa yaliyo na msingi wa lugha bado wataripoti kwa mafunzo ya kibinafsi, kama ilivyopangiwa awali siku ya Alhamisi, Septemba 17 kwa siku ya kwanza ya shule.
- Wanafunzi katika madarasa ya 1-12 (ambao hawajapangiwa kwa programu ya masomo maalum iliyo tofauti zaidi na masomo ya kawaida) ambao walikuwa wamepangiwa kwa mafunzo ya kibinafsi wataanza mwaka wa shule katika mazingira ya mafunzo ya mbali. **Familia watajulishwa kuhusu tarehe ya kuanza upya kwa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi darasani kwa wanafunzi hawa.**
- Wanafunzi wa chekechea ya awali na chekechea, ambao walipata nafasi ya kuhudhuria darasani kibinafsi bado wataripoti kibinafsi shuleni kwao, kama ilivyopangiwa, awali siku ya Jumatatu, Septemba 21 kwa siku yao ya kwanza shuleni.
- Wanafunzi wote waliopangiwa kusoma katika mafunzo ya mbali wataendelea kama ilivyopangiwa awali.

Ninaelewa namna hili linaweza kusumbua na kusikitisha kwa familia. Kabla ya kuchukua uamuzi huu, tumejaribu chaguo zingine zote – za kimtaa na kitaifa – za kupata vifaa vya kusafisha hewa tunazohitaji kama sehemu ya itifaki yetu ya kuzidisha miongozo ya kiafya na usalama zinazohitajika ili kufungua upya madarasa. Mwishowe, sisi tulichukua ahadi kuweka usalama wa mwanafunzi na mfanyikazi kama kipaumbele cha juu zaidi, na tunashikilia ahadi hii.

Katika kupangilia mwaka wa shule mpya, tulijitayarisha kwa uwezekano kama huu, na tuko tayari kubadilisha kwa muda mfupi na kuendelea na mafunzo ya mbali kote wilayani kwa wanafunzi walioorodheshwa hapa juu na kuendelea na mpango wa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi baada ya kufuatilia nokta za data zinazohusika na COVID-na kupata kwa kikamilifu vifaa vya usalama na usafishaji.

Ili kupangilia kwa Alhamisi, unaweza kutarajia kuwasiliwa moja kwa moja na shule yako kuhusu mpango wake wa kibinafsi kuhusu siku ya kwanza ya kuhudhuria mafunzo ya mbali ya mtoto wako. Unaweza pia kutarajia arifa kuhusu huduma ya chakula na usambazaji wa vifaa vya mafunzo ya mtandao.

Asante kwa uwezo wako kubadilika kirahisi na ufahamu wako tunavyotarajia kuanza mwaka wa shule katika mbinu yenye usalama zaidi kwa wanafunzi wetu na wafanyikazi wetu wote.

Wako Mwaminifu,

Dr. Joel D. Boyd
Msimamizi wa Mashule